# MAFUNDISHO YA MSINGI NA ZAIDI

Mwongozo wa Somo la Biblia

# MAFUNDISHO YA MSINGI NA ZAIDI

## Mwongozo wa Somo la Biblia

Imeandikwa na Bob Waliszewski

**Mafundisho Ya Msingi Na Zaidi**
Mwongozo wa Somo la Biblia

Imeandikwa na Bob Waliszewski
Imetafsiriwa na Tegemea Mbise
Imehaririwa na Nkongi Emmanuel Kamwela na Esta Kweka

Imechapishwa na Foursquare Missions Press © 2003
Pamoja na Mizizi Mobile Missions Press © 2022

# YALIYOMO


| Sura | | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1. | Neno | 5 |
| 2. | Mungu | 8 |
| 3. | Yesu | 12 |
| 4. | Roho Mtakatifu | 15 |
| 5. | Dhambi | 17 |
| 6. | Kuzaliwa Mara ya Pili | 20 |
| 7. | Ubatizo wa Maji | 23 |
| 8. | Ubatizo wa Roho Mtakatifu | 26 |
| 9. | Sifa | 29 |
| 10. | Maombi | 31 |
| 11. | Imani | 34 |
| 12. | Uzima Tele | 37 |
| 13. | Uponyaji wa Kimungu | 39 |
| 14. | Kurudi Mara ya Pili | 42 |
| 15. | Hukumu | 45 |

## SURA YA 1
# NENO

Biblia, Neno la Mungu, ndio msingi wetu wa kumjua Mungu. Kujaribu kumjua Mungu bila hilo ni kama kujaribu kujenga nyumba bila kuwa na ramani. Biblia ni ramani yetu kwa ajili ya maisha. Inayo maelezo jinsi ambavyo Mungu anamjali mwanadamu. Ni barua ya upendo ya Mungu kwa mwanadamu.

Biblia ni kweli kabisa na sahihi. Iliandikwa na watu ambao walivuviwa na Mungu. Hakuna kitabu kingine kinachoweza kufikia Biblia kwa umuhimu au ubora. Ni mwongozo wa maisha ya mwamini, wa milele na sasa. Mkristo ambaye imani yake inakua ni yule anayeamini Biblia na ambaye anachukua muda kila siku kusoma na kujifunza Neno.

1. Je! Yesu alifikiri nini kuhusu Agano la Kale? (Mathayo 4:4,7,10) ______________________

   ______________________

   ______________________

   ______________________

2. Watu wengine hujaribu kupunguza visa vya Biblia kuwa hadithi na hekaya tu. Yesu aliwaonaje? (Mathayo 12:40)

   ______________________

   ______________________

3. Biblia inajithibitisha yenyewe kuwa kweli. Ni kiasi gani Biblia ni ya kuaminika? (2 Timotheo. 3:16; 2 Petro 1:20, 21) ______________________

   ______________________

4. Mengi yanaweza kusemwa juu ya uvuvio wa Agano la Kale, lakini vipi kuhusu Agano Jipya? Je! Petro anasema nini juu ya nyaraka za Paulo? (2 Petro 3:15-16) ______

______

______

5. Je! Biblia inasemaje juu ya ukweli wa maneno ya Kristo kama ilivyoandikwa katika Injili nne? (Yohana 6:63; Yohana 17:8) ______

______

6. Je! Unaweza kupata faida gani kupitia Neno la Mungu? (2 Timotheo 3:16) ______

______

7. Kulitafakari neno la Mungu ni zaidi ya kulisoma. Ni kusoma na kusoma tena, kukariri na kulitendea kazi. Je! Kuna faida gani za ziada kwako katika aina hii ya kujifunza? (Yoshua 1:8) ______

______

______

8. Ujuzi wa akili tu wa Neno la Mungu hautoshi-inatakiwa kuliamini. Je! Ni mtu gani aliyejua Maandiko vizuri ambaye Yesu alisema naye, Mathayo 4:1-11 hii ndiyo inaonyesha hili kwa wazi kabisa? ______

______

______

9. Ni njia gani zimetajwa katika Wakolosai 3:16 kwa ajili ya mtu anayeamini ili Neno likae ndani yake?

________________________________________

________________________________________

Orodhesha mawazo mengine.____________________

________________________________________

________________________________________

10. Je! Yakobo anasema nini kuhusu mwamini na Neno? (Yakobo 1:22)______________________________

________________________________________

11. Je! Kuna matumizi gani ya Neno tunapolifikiria kama upanga? (Waebrania 4:12) ______________________

________________________________________

12. Toa mfano wa matumizi ya Neno kama upanga.

________________________________________

________________________________________

# SURA YA 2
# MUNGU

Mungu ni Mungu. Siku zote amekuwepo na atakuwepo kila wakati. Kwa kupitia yeye vitu vyote viliumbwa. Nguvu na maisha vinatoka kwake. Yeye ni Mwenye enzi. Ni mwenye nguvu zote. Yeye anajua yote. Na bado, Yeye ni mwenye upendo. Lakini haijalishi tunajaribu sana, hatuwezi kumuweka Mungu ndani ya "kisanduku." Yeye ni mkubwa sana. Ni jinsi gani basi tunaweza kumchunguza? Tunaweza kumchunguza Mungu kupitia Mwanae Yesu Kristo. (Wakolosai 2:9 "Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.")

Kumwelewa Mungu kikamilifu haiwezekani. Mungu anazidi ufahamu wa mwanadamu. Hata hivyo mengi juu ya Mungu yanaweza kueleweka kwa sababu Mungu alichagua kujifunua kwa mwanadamu.

1. Soma Mwanzo 1:1 (maneno manne ya mwanzo tu) na hujibu swali: Nini dhana ya msingi kuhusu asili ya milele wa Mungu inayopaswa kuaminiwa ili kuelewa zaidi kuhusu yeye? (Tazama pia Kumbukumbu la Torati 33:27; Mika 5:2; Kutoka 3:14) ____________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

2. Soma Mwanzo 1:1. Ni ufahamu gani kuhusu asili ya Mungu unaupata kwenye aya hii?

   ______________________________________________

   ______________________________________________

3. Je! Biblia inafundisha nini kuhusu Mungu katika maandiko yafuatayo: Kumbukumbu la Torati 6:4; 1 Mambo ya Nyakati 16:26; 1 Wakorintho 8:4-6? ________

________________________________________

________________________________________

4. Mungu amefunua nyanja nyingi za utu wake kwa kupitia Neno Lake. Ni ufahamu gani unaweza kupata kutoka katika maandiko yafuatayo:

   1 Wakorintho 10:13
   Kutoka 34:6,7
   Zaburi 91:1,2
   Zaburi 121:3,4
   Zaburi 103:17
   Zaburi 34:8
   Zaburi 23:2,3
   Mambo ya Walawi 19:2
   Zaburi 18:30
   Hesabu 23:19
   Isaya 55:8

5. Je! Mungu ametuita tuwe na nafasi gani katika Kristo? (Warumi 8:15; 1 Yohana 3:1)________________________

________________________________________

6. Vile tunavyojua sivyo Mungu anavyojua. Ni kwa nini? (Matendo 15:18; Mathayo 6:8; Yeremia 1:5) ___________

________________________________________

7. Je! Mungu ni mkubwa kiasi gani? (1 Wafalme 8:27) ____

_______________________________________________

8. Kwa nini hakuna mtu aliyewai kumwona Mungu? (Yohana 4:24; 1 Timotheo 1:17) ___________________

_______________________________________________

9. Sifa moja ya Mungu ni madai yake kuwa Mungu "mwenye wivu". (Kutoka 20:5; Kumbukumbu la Torati 4:24). Je! Hii kwako ina maanisha nini?_____________

_______________________________________________

10. Je! Tunaweza kupata hakika gani ya kumjua Mungu kupitia maandiko haya:
    1 Mambo ya Nyakati 28:9 ______________________
    Zaburi 139:1-4______________________________
    Mathayo 10:30 ______________________________

11. Je! Kuna kitu chochote ambacho Mungu hawezi kufanya? (Mathayo 19:26) _______________________

_______________________________________________

12. Mungu anadhibitije uovu? (Mwanzo 50:20; Warumi 8:28) _____________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

13. Yesu alisema Mungu alikuwa mtoaji. Kwa nini? (Yohana 3:16; 1 Yohana 4:8) ______________________

______________________________________________

14. Je! Yohana1:1; Matendo 5:3, 4 na Kumbukumbu la Torati 6:4 inatufundisha nini kuhusu Mungu? __________

______________________________________________

______________________________________________

## SURA YA 3
# YESU

Vitu vingi maishani vinaweza kugawanywa katika asilimia. Mgongo wa shati lako una lebo ambayo inasomeka kitu kama hiki: pamba 50%, polyester 50%. Ikiwa Yesu angekuwa na lebo, ingekuwa lebo hisiyokuwa ya kawaida zaidi ulimwenguni. Maandishi yake yangesoma 100% Mungu - 100% mwanadamu.

1. Agano la Kale lilitabiri mambo mengi juu ya maisha ya Kristo karne kadhaa kabla ya kuzaliwa kwake. Je! Mika anatabiri nini juu ya kuzaliwa kwa Kristo? (Mika 5:2)

   ________________________________________

   ________________________________________

2. Je! Isaya 7:14 ilitimizwaje katika kuzaliwa kwa Kristo?

   ________________________________________

   ________________________________________

3. Kwa nini Yesu alibatizwa? (Mathayo 3:15) ____________

   ________________________________________

   Ona Utatu huo katika aya ya 16-17.

4. Huduma za Yesu duniani zilikuwa nyingi. Kwa kutumia maandiko yafuatayo, orodhesha kadhaa.
   - Mathayo 4:17
   - Mathayo 5:2
   - Mathayo 8:16
   - Mathayo 8:23-26
   - Luka 5:24
   - Luka 7:14, 15
   - John 3:17

5. Ni muhimu sana kuelewa kuwa Yesu alikuwa 100% binadamu. Mara nyingi alikuwa amechoka. Alihisi kukataliwa, na alihisi majaribu bado bila dhambi. Kwa kweli, Yesu anaweza kuelewa kila kitu tunapitia kwa sababu amekwisha kupitia. Je! Ni sifa gani za kibinadamu tunazoziona katika Yesu?

   Yohana 11:35 ______________________________

   Luke 8:23 ______________________________

   Marko 6:30-34 ______________________________

   Waebrania 4:15 ______________________________

   Yohana 19:1-3 ______________________________

   Wafilipi 2:8 ______________________________

6. Ni muhimu kabisa pia kuelewa kwamba Yesu alikuwa 100% Mungu. Je! Tomaso alimwambia Yesu nini juu ya Uungu wake? (Yohana 20:26-29) ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

7. Petro alisema Kristo alikuwa nani? (Mathayo 16:16)

   ______________________________

8. Je! Yohana Mbatizaji alisema Yesu alikuwa nani? (Yohana 1:29-34) ______________________________

   ______________________________

9. Malaika ambaye alizungumza na wachungaji alisema nini kuhusu Yesu? (Luka 2:11) ______________________________

   ______________________________

   Kwa habari zaidi tazama pia taarifa ya Simioni na Anna juu ya Yesu (Luka 2:25-38).

10. Ni yapi madai ya Yesu juu yake mwenyewe?

Yohana 8:58

Marko 2:7-10

Yohana 18:37

Yohana 10:30, 33

Yohana 9:35-38

Yohana 5:18

11. Yesu alikuwa wapi kabla Ajazaliwa na Mariamu? (Yohana17:5, 24) ______________________________

______________________________________________

12. Je! Jukumu la Kristo lilikuwa lipi wakati wa uumbaji? (Wakolosai 1:15,16; Yohana 1:1-3) ________________

______________________________________________

13. Je! Ni ipi nafasi ya Kristo mbinguni kuhusiana na malaika? (Waebrania 1:4, 6) ______________________

______________________________________________

14. Ni nani aliyemwona Kristo baada ya kufufuka kwake? (1 Wakorintho 15:5-8) _________________________

______________________________________________

15. Ni tukio gani la kihistoria lililotokea ambalo lilifanya Kristo asiwe tena na sisi kimwili? (Matendo 1:9) _____

______________________________________________

16. Je! Malaika waliahidi nini kuhusu Kristo katika Matendo ya Mitume 1:11? ______________________________

______________________________________________

## SURA YA 4
# ROHO MTAKATIFU

Roho Mtakatifu ndiye mmojawapo wa Utatu. Yeye sio nguvu ya ulimwengu au "icho." Yeye ni tofauti na Baba na Mwana, lakini bado Utatu huo ni kamili na mmoja kabisa.

1. Roho alikuwa wapi wakati wa uumbaji? (Mwanzo 1:2)

   ______________________________

2. Je! Roho Mtakatifu alichukua jukumu wakati wa Agano la Kale? (Zaburi 51:11) ______________________________

   ______________________________

3. Kulingana na Mathayo 28:19, je! Roho Mtakatifu ni sawa katika maumbile na Baba na Mwana?

   ______________________________

   ______________________________

4. Je! Ni sifa gani binafsi zilizowekwa kwa Roho Mtakatifu?

   Warumi 8:27 ______________________________

   1 Wakorintho 2:10, 11 ______________________________

   Warumi 15:30 ______________________________

   1 Wakorintho 12:4-11 ______________________________

   Waefeso 1:17-20 ______________________________

   Yohana 16:13 ______________________________

5. Ni zipi njia kadhaa ambazo Roho Mtakatifu anaweza kuathiriwa nazo binafsi?

    Isaya 63:10 ______________________________

    Waefeso 4:30 ______________________________

    Waebrania 10:29 ______________________________

    Matendo 5:3 ______________________________

    Mathayo 12:31, 32 ______________________________

6. Kwa nini Yesu alipanda kwenda kwa Baba yake? (Yohana 16:5-7) ______________________________

    ______________________________

7. Je! Roho Mtakatifu anakaa wapi? (1 Wakorintho 6:19)

    ______________________________

    ______________________________

8. Je! Ni huduma gani za Roho Mtakatifu?

    1 Wakorintho 12:4-11 ______________________________

    Wagalatia 5:22 ______________________________

    Matendo 1:5-8 ______________________________

    Warumi 8:26 ______________________________

9. Soma Matendo 5:3, 4. Ni nini kinachoweza kujifunzwa kuhusu Roho Mtakatifu kupitia maandiko haya? ________

    ______________________________

SURA YA 5

# DHAMBI

Dhambi ni kitu chochote mtu hufanya au hafanyi kinyume na mpango wa Mungu. Dhambi imesababisha kizuizi kati ya Mungu na mwanadamu (Isaya 59:2), kizuizi ambacho Yesu Kristo pekee ndiye anayeweza kuunganisha. Mungu hakuumba dhambi - mwanadamu alichagua kutenda dhambi na kwa kufanya hivyo alimwasi Muumba wake. Adhabu ya uasi huu ni mauti ya milele (Warumi 6:23). Ashukuriwe Mungu kwamba kwa kumwamini Kristo tumevuka kutoka mautini kwenda uzimani. (Yohana 5:24)

1. Baada ya Mungu kuumba mwanadamu na ulimwengu wake, lengo lake lilikuwa lipi kuhusu vyote viwili? (Mwanzo 1:31)

   ______________________________

   ______________________________

2. Je! Dhambi ilianza lini? (Yuda 1:6; 2 Petro 2:4) ________

   ______________________________

   ______________________________

3. Je! Ni amri gani ya Mungu kwa Adamu kuhusu miti na matunda yake? (Mwanzo 2:16, 17)

   ______________________________

   ______________________________

4. Soma Mwanzo 3:1-6.
   a. Je! Hawa alifanya dhambi gani? ____________
   b. Je! Kwa nini Hawa alifanya dhambi? ____________
   c. Matokeo yalikuwa nini? ____________

5. Soma Warumi 5:12-17. Adamu alikuwa na athari dhahiri ya kihistoria.
   a. Ni athari gani?____________
   b. Namna gani tatizo hili linaweza kutatuliwa?____________

   ____________

6. Je! Kuna vitendo ambavyo kwa mtu mmoja vinaweza kuwa dhambi, lakini kwa mtu mwingine iwe sahihi kabisa? (Warumi 14:1-3) ____________

   ____________

7. Je! Ufafanuzi wa Paulo kuhusu dhambi ni nini katika Warumi 14:23? ____________

   ____________

8. Soma 1 Yohana 1:8 - 1 Yohana 2:2.
   a. Mtazamo wa Mkristo unapaswa kuwa nini juu ya dhambi? ____________

   ____________

   b. Je! Wakristo wanahitaji kufanya nini ili kupata msamaha wa dhambi?____________

   ____________

9. Soma 1 Yohana 3:4-6. Eleza kutokubaliana kwa dhahiri kati ya maandiko haya na 1 Yohana 2:1. ______________

______________________________________________

10. Je! Daudi alisema nini juu ya dhambi na ni nani hatimaye inathiri? (2 Samweli 12:13) ______________

______________________________________________

11. Je! Mungu "hufanya nini juu ya dhambi Mkristo anayotenda? (Zaburi 103:12) ______________________

______________________________________________

______________________________________________

## SURA YA 6
# KUZALIWA MARA YA PILI

Sisi sote tulizaliwa idadi ya miaka kadhaa iliyopita bila kuchagua sisi wenyewe. Wazazi wetu walifanya chaguo hilo. Kristo alitaka kila mtu apate kuzaliwa kiroho ili kuwa mshiriki wa familia ya Mungu. Kuzaliwa huku hakutegemei kitu chochote zaidi ya kukiri kwetu, kujitolea na kukubali kuwa Yeye ni Bwana (Warumi 10:9, 10). Kazi, matendo, na mwenendo haviathiri chochote, wala historia yetu ya dhambi ya zamani. Muuaji mbaya zaidi anaweza kuzaliwa upya sawasawa kabisa na mtu asiye na hatia katika ulimwengu wote. Kwa maana hata mtu asiye na hatia kabisa bado ana dhambi. Wote wamefanya dhambi na kwenda kinyume na matakwa ya Mungu hivyo wote wanahitaji kupata kuzaliwa kiroho ili kuwa katika umoja na Mwenyezi.

1. Soma Yohana 3:1-21. Je! Yesu alimwambia Nikodemo nini juu ya vigezo vya kuona Ufalme wa Mungu? ______

   ________________________________________

2. Je! Unaaminije mtu kazaliwa tena? ____________________

   ________________________________________

3. Je! Jitihada zina mchango gani katika kuzaliwa mara ya pili? (Waefeso 2:8,9) ______________________________

   ________________________________________

   (1 Wakorintho 3:11-15) ___________________________

   ________________________________________

4. Matokeo ya dhambi ni nini? (Warumi 6:23) __________

5. Baada ya kuwa Mkristo, je! Mtume Paulo bado alipambana na dhambi? (Warumi 7:14-20) ____________

____________________________________________

____________________________________________

6. Ni nini kinachotokea juu ya "Hukumu ya laana" kwa waumini waliozaliwa mara ya pili? (Warumi 8:11) ______

____________________________________________

7. Ni nini kinachotokea wakati mtu anapata kuzaliwa upya katika Kristo?
(2 Wakorintho 5:17) ____________________________

____________________________________________

(2 Wakorintho 5:21) ____________________________

____________________________________________

8. Soma Warumi 10:9,10. Kwa nini unafikiri kwamba Paulo alisema ni muhimu kumkiri Yesu kwa kinywa chako? ________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

9. Yesu hatajilazimisha kwa mtu. Jinsi gani Ufunuo 3:20 inaelezaje jambo hili?

____________________________________________

____________________________________________

10. Je! Ni nini athari au matokeo katika maisha ya mtu baada ya kubadilika?

Yohana 3:18a ______________________________

Matendo 8:8 ______________________________

Warumi 5:1 ______________________________

2 Wakorintho 6:16-18 ______________________

Warumi 8:15 ______________________________

11. Wokovu unadhihirisha asili iliyobadilishwa kulingana na 2 Wakorintho 5:17. Na hii ni wazi kufuatana na:

1 Yohana 3:19 ______________________________

1 Yohana 4:7 ______________________________

1 Yohana 5:4 ______________________________

S U R A  Y A  7

# UBATIZO WA MAJI

Bwana aliwaamuru wanafunzi wake kutunza maagizo mawili (maadhimisho mawili ya nje) ambayo yalipangwa kuwa baraka na msaada kwao katika maisha yao ya Kikristo na huduma. Moja lilikuwa Ubatizo wa Maji na lingine la Meza ya Bwana.

Ubatizo wa Maji ni sehemu muhimu ya Ukristo. Nyumba ya Kornelio, jamaa na marafiki wote walibatizwa kwa maji (Matendo 10:47, 48). Towashi wa Kushi alibatizwa mara moja baada ya kubadilika kwake (Matendo 8:36-38).

1. Ubatizo wa Maji ni ishara ya nje ya kazi ya ndani. Elezea Luka 3:3. ____________________

   ____________________

2. Soma Warumi 6:1-4

   a. Wakristo hubatiziwa katika nini? ____________________

   ____________________

   b. Je! Hiyo inamaanisha nini kwako? ____________________

   ____________________

   c. Ni nini hutokea wakati wa ubatizo? ____________________

   ____________________

   d. Matokeo ya kubatizwa yanapaswa kuwa nini? ____________________

   ____________________

3. Je! Ni amri gani ambayo Kristo alitoa juu ya ubatizo ambayo inaonyesha wazi umuhimu wake na faida zake? (Mathayo 28:19)______________________________

__________________________________________

__________________________________________

4. Je! Paulo na Yohana walisema nini ambacho kinakuongoza kuamini kwamba wokovu na ubatizo wa maji ni vitu viwili tofauti?
   a. Waefeso 2:8 ______________________________
   b. Waebrania 9:22 ____________________________
   c. 1 Yohana 1:7 ______________________________

5. Yohana Mbatizaji hakuwa mtu pekee wa kubatiza. Angalia watu ambao walihusika katika kubatiza katika maandiko yafuatayo:
   a. 1 Wakorintho 1:13-16 ______________________
   b. Matendo 8:38 _____________________________
   c. Yohana 4:1, 2 _____________________________

6. Ingawa Wakristo wote wanapaswa kubatizwa, wakati mwingine ubatizo hauwezekani-kama vile ubadilishaji wa kitanda cha kifo. Je! Yesu anasema nini inaonyesha kwamba wokovu hautegemei ubatizo wa maji? (Luka 23:39-43) ___________________________________

__________________________________________

__________________________________________

7. Soma Mathayo 3:13-17.

a. Kwa nini Yohana hakutaka kumbatiza Yesu? ___________

_______________________________________________

b. Kwa nini Yesu alibatizwa? ___________________________

_______________________________________________

c. Jinsi gani Yohana alimbatiza Yesu? __________________

_______________________________________________

8. Ni nani anayeweza kubatizwa? (Matendo 16:25-34)

_______________________________________________

_______________________________________________

9. Yesu hakubatizwa akiwa mtoto mchanga. Kwa nini? Kwa nini basi, alipelekwa Hekaluni? (Luka 2:21-24)

_______________________________________________

_______________________________________________

## SURA YA 8
# UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU

Siku moja wakati Yohana Mbatizaji alikuwa akibatiza, alimwona Yesu na kuwaambia watu kuwa Yesu ni nani. Kwanza, alielezea kwamba Yesu alikuwa ni Mwana-kondoo wa Mungu ambaye angeondoa dhambi za ulimwengu na kwamba (Yesu) atabatiza kwa Roho Mtakatifu (Yohana 1:29-34).

Mara tu kabla ya kupaa, Kristo alisema maneno ya Yohana na aliwaahidi wanafunzi wake kwamba watabatizwa na Roho Mtakatifu (Matendo 1:4-8).

Kuna kitu kilikosekana katika maisha ya wanafunzi na Kristo alikijua. Ingawa wanafunzi wake walikuwa waumini waliojitoa, Kristo aliwaamuru kutokwenda nje na kuhudumu kwa kuwa walikuwa hawajapokea kipawa ambacho kingewapa nguvu; na hicho kipawa kilikuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

1. Ni nabii gani katika Agano la Kale alitabiri ubatizo wa Roho Mtakatifu? (Yoeli 2:29) ________________________

   ________________________________________________

2. Ni mwanafunzi gani aliyezungumzia utimilifu huu na ilikuwa iwe kwa wakati gani? (Matendo 2:14-16)

   ________________________________________________

   ________________________________________________

3. Je! Matukio ya Matendo 8:1-17 yanaonyeshaje kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tofauti na ile ya uzoefu wa kuzaliwa mara ya pili? ____________________

____________________

4. Je! Biblia inasema nini juu ya mtu anayeenenda katika Roho? (Wagalatia 5:16) ____________________

____________________

5. Soma Matendo 2:1-4. Ingawa wanafunzi walikuwa na Roho aliyeishi ndani yao, hawakujazwa au kubatizwa na Roho.

   a. Je! Ni lini wanafunzi walipokea uzoefu huu wa pili, ubatizo na Roho Mtakatifu ambao Kristo alikuwa ameahidi? ____________________

   ____________________

   b. Je! Ni ishara gani za nje zilizoifanya iwe wazi kuwa wanafunzi walibatizwa kwa Roho Mtakatifu? __________

   ____________________

6. Mahubiri ya Petro siku ya Pentekoste yalionyesha wale ambao wanaweza kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Je! Petro alisema ni nani angepokea? (Matendo 2:36-39)

____________________

____________________

7. Kwa nini wanafunzi walihitaji kipawa cha kubatizwa na Roho Mtakatifu? (Luka 24:49; Matendo 1:8) __________

________________________________________

8. Maandiko yafuatayo yanahusu matukio mengine ambapo watu walibatizwa kwa Roho Mtakatifu. Baada ya kuangalia maandiko utaandika mhusika na ni ishara gani, iliyofuatana na kila tukio.
   a. Acts 8:14-17 ______________________________
   b. Matendo 9:10-19 ___________________________
   c. Matendo 10:39-48 (Ona kwamba ubatizo wa maji na ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tofauti.) __________

      ________________________________________
   d. Matendo 19:1-7 ____________________________

9. Je! Mtu lazima afanye nini ili abatizwe na Roho Mtakatifu? (Luka 11:9-13) ___________________________

________________________________________

________________________________________

## SURA YA 9
# SIFA

Sifa ni sehemu muhimu ya mwitikio wa Mkristo kwa Mungu. Ni kumjulisha Mungu kupitia sala kwamba mtu anathamini Muumba wake na mambo ambayo Amefanya na Anayoendelea kufanya katika maisha yake. **Sifa ni nini?**

1. Soma Luka 17:11-19.

   a. Je! Watu wengi waliitikiaje baada ya kuponywa kupitia Kristo? ______________________________

   ______________________________________________

   b. Je! Yule mwenye ukoma alijibuje? ________________

   ______________________________________________

2. Mtu anapaswa kumsifu Mungu mara ngapi? (Waefeso 5:19, 20; Zaburi 92:2) _________________________

   ______________________________________________

3. Mtu anaweza kumsifu Mungu katika njia gani?

   a. Waefeso 5:19, 20 __________________________
   b. Zaburi 150 _______________________________
   c. 1 Wakorintho 14:13-16 _____________________

4. Kwa nini mtu anapaswa kumsifu Mungu?

   a. 2 Samweli 22:4 ____________________________
   b. Zaburi 92:1 ______________________________
   c. Zaburi 145:3-9 ____________________________

5. Soma Matendo 16:16-34.
   a. Kwa nini Paulo na Sila waliwekwa jela? ____________

   ______________________________________________

   b. Licha ya kutupwa gerezani, ni unyanyasaji gani ambao Paulo na Sila walipata? ____________________

   ______________________________________________

   c. Je! Majibu yao yalikuwaje kwenye mateso yao? _____

   ______________________________________________

   d. Je! Matokeo ya ushuhuda wa Paulo na Sila yalikuwa nini kwa mlinzi wa gereza? ____________________

   ______________________________________________

6. Je! Habakuki alisema nini juu ya sifa katika sala yake? (Habakuki 3:3) ____________________________________

   ______________________________________________

7. Waumini wapaswa waje namna gani mbele ya uwepo wa Bwana? (Zaburi 100:4) ____________________

   ______________________________________________

8. Je! Petro anamaanisha nini anaposema juu ya sifa katika 1 Petro 1:7? ______________________________

   ______________________________________________

9. Orodhesha njia kadhaa za vitendo ambazo unaweza kumsifu Mungu maishani mwako. ____________________

   ______________________________________________

## SURA YA 10
# MAOMBI

Maombi ni mazungumzo tu na Mungu. Haipaswi liwe jambo la kudhania. Sio lazima kuwa ya muda mrefu au sahihi kisarufi. Maombi yanaweza kuwa kwa Kiingereza, Kihispania, Kiebrania au hata lugha elfu tofauti. Kwa maana Mungu anajua tunayohitaji hata kabla ya kuomba. (Mathayo 6:8)

1. Soma Luka 11:1-13. Maombi ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi wake katika mistari ya 2-4 ni mwongozo mzuri wa maombi kwa jumla. Je! Ni miongozo gani katika maombi haya unaoweza kukufaa katika maombi yako mwenyewe? ______________________________

   ______________________________________________

2. Je! Habari kuhusu jirani anayeuliza mkate hufundisha nini kuhusu sala?______________________________

   ______________________________________________

3. Unapaswa kusali mara ngapi? (1 Wathesalonike 5:17)

   ______________________________________________

   ______________________________________________

4. Katika macho ya Mungu, yeye anakuonaje ikiwa hautamwombea mtu ambaye unajisikia kumwombea au unalemewa naye? (1 Samweli 12:23) ______________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

5. Tunapaswa kusali vipi?
   a. Mathayo 6:6 ____________________
   b. Waebrania 4:16 ____________________
   c. Mathayo 18:19 ____________________
   d. Marko 11:24 ____________________
   e. Yakobo 5:16 ____________________
   f. Zaburi 37:4 ____________________

6. Je! Kwa nini maombi yote hayajibiwa kwa njia tunavyofikiria inapaswa kuwa?
   a. Isaya 55:8 ____________________
   b. 2 Wakorintho 12:8 ____________________
   c. Mathayo 6:7 ____________________
   d. Daniel 10:12-14 ____________________
   e. 1 Petro 3:7 ____________________

7. Soma 1 Timotheo 2:1. Ushirika na Mungu kwa kiasi kikubwa ni ibada, kuadhimisha na sifa. Je! Paulo anamhimiza Timotheo afanye nini?
   a. ____________________
   b. ____________________
   c. ____________________
   d. ____________________

8. Paulo anazungumza juu ya hitaji la maombi katika huduma ya Kikristo. Katika maandiko yafuatayo, sala huombwa kwa nani?

   a. Matendo 6:4 ________________________________

   b. Mathayo 17:21 ______________________________

   c. Matendo 12:5 _______________________________

   d. 2 Wakorintho 1:11 ___________________________

## SURA YA 11
# IMANI

Ufunguo wa kufungua kila siri katika Biblia hutokana na "imani." Imani ni zaidi ya ufahamu wa kiakili, ni ujasiri kamili na tumaini pale mtu anajitoa kwa kitu kabisa. Kuna hadithi ya mtu ambaye alitembea kwenye kamba juu ya maporomoko ya maji wa mto wa Niagara akisukuma toroli iliyojaa matofali. Alifanya safari hiyo mara kadhaa - akisukuma toroli huku wakati akienda mbele na kuvuta toroli akienda nyuma. Mwishowe, alisimama muda wa kutosha kuongea na umati wa waliokuwa wakimwangalia. Akauliza, "Je! Kuna mtu yeyote anayeamini kwamba ningeweza kuchukua matofali haya kutoka kwenye toroli hili na kumtia mtu ndani yake ninapotembea kwenye kamba juu ya maporomoko ya maji?" Umati wote ulikubali. Basi yule mtembea kwa kamba aliuliza tena, "Nani angependa kuwa wa kwanza kujitolea?" Alitazama na kungojea, hakuna mtu aliyejitolea. Kwa kweli, hakuna mtu aliyeamini hadi kufikia kile ambacho Biblia huita imani. Imani ya kweli ilikosekana kwani hakuna mtu ambaye kwa kweli "angejitoa" hadi kufikia hatua ya kuingia kwenye toroli.

1. Imani ni nini kwako? ______________________________

   ______________________________

2. Je! Biblia inasema nini juu ya imani?
   (Waebrania 11:1-3) ______________________________

   ______________________________

3. Katika dhiki zote za Ayubu, imani yake tu ndio iliyomwimarisha. Kwa nini Ayubu alikuwa na imani? (Ayubu 13:15,16; Ayubu 19:25,26) ____________________

________________________________________

4. Kwa nini unapaswa kuwa na imani? (Wafilipi 4:6; Habakuki 3:17-19) ____________________

________________________________________

5. Wakati mwingine inaonekana kwamba imani yetu inajaribiwa. Ni nini hasa kinachotokea wakati huu? (Yakobo 1:2, 3) ____________________

________________________________________

6. Mtu anahitaji kuwa na imani kiasi gani? (Mathayo 17:20; Mithali 3:5) ____________________

________________________________________

7. Matokeo ya imani ya kimungu ni nini? (Warumi 8:28)

________________________________________

________________________________________

8. Imani inashika sehemu muhimu ya silaha ya Mungu. Toa umuhimu wake. (Waefeso 6:16) ____________________

________________________________________

9. Ni nini kinachoweza kuharibu imani ya mtu? (Warumi 8:37-39) ____________________

________________________________________

10. Tunapaswa kufanya nini ikiwa tunahisi kwamba imani yetu haitoshi? (Marko 9:24) ____________________

____________________________________________

11. Imani yetu inapaswa kukaa wapi na matokeo ya imani ya aina hii ni yapi? (Warumi 3:21-26) ____________

____________________________________________

12. Mungu ni Mpaji wetu na Chanzo chetu. Anatuamuru tusiwe na wasiwasi juu ya kitu chochote, lakini kuwa na imani kila wakati. Je! Mwelekeo wako maishani unapaswa kuwa wapi? (Mathayo 6:33) ____________

____________________________________________

____________________________________________

SURA YA 12
# UZIMA TELE

Katika ukristo, wakati unaishi kikamilifu kama Mungu anavyokusudia inafurahisha, inatia nguvu na kuleta maana bora. Yesu alisema kwamba alikusudia watoto wake wote wapate furaha ya kweli (Yohana 17:13). Kwa kweli, hata aliomba kwamba Wakristo wote wapate "kipimo kamili cha furaha" ambacho Yeye atakitoa. Hii inaanza wakati wa wokovu, lakini haishii hapo. Kwa maana Mungu anakusudia tuingie katika rasilimali Yake ili tupate maisha kwa kiwango kikamilifu katika maisha yetu.

1. Soma Yohana 10:10.
   a. Mwizi ni nani? ______________________________
   b. Lengo la mwizi ni nini? ______________________
   c. Lengo la Mchungaji Mwema ni nini? ____________

2. Swali la kufikiria: Yesu alikuwa mtu wa furaha ya kweli, lakini bado alipata maumivu. Alilia na alikasirika hadi akafukuza wabadilishaji wa pesa Hekaluni. Je! Kuna tofauti kati ya furaha na shangwe? ________________

   ____________________________________________

3. Je! Ni nini matakwa ya Mungu kwa mwamini kuhusu furaha? (Wafilipi 4:4) __________________________

   ____________________________________________

4. Paulo alikuwa wapi wakati aliandika andiko lifuatalo? (Wafilipi 1:12,13)

   ____________________________________________

5. Ni rahisi kupata furaha wakati wa hali nzuri. Lakini unawezaje kupata furaha wakati usio wa hali nzuri?
   a. Yakobo 1:2 ______________________________
   b. Warumi 8:28 ______________________________
   c. 1 Wathesalonike 5:16-18 ______________________

6. Maisha mengi ya Kikristo hayapatikani na "watoto wachanga katika Kristo." Soma Waebrania 5:1–6:3.
   a. Je! Mkristo anapaswa kukusudia nini kuhusu ukuaji wake binafsi? ______________________________

   ______________________________________________

   b. Mtu hufikiaje lengo hili? ______________________

   ______________________________________________

7. Uzima tele ni maisha ya ushindi. Soma Waefeso 6:10-18.
   a. Je! Kwa nini Mkristo anapaswa kuvaa silaha za Mungu? ______________________________________

   ______________________________________________

   b. Ni silaha ngapi za Mungu zinahitajika kupigana vita vizuri kiroho? ______________________________

   ______________________________________________

   c. Orodhesha silaha za ulinzi za Mungu: __________

   ______________________________________________

   d. Ni silaha ipi tu iliyotengenezwa kwa kupigana vita?

   ______________________________________________

   ______________________________________________

SURA YA 13

# UPONYAJI WA KIMUNGU

Ukweli wote wa Agano Jipya una mizizi yake katika Agano la Kale. Agano la Kale na Jipya hutoa agano la uponyaji la kimungu. Isaya anatabiri juu ya huduma ya uponyaji ya Kristo, na Yesu mwenyewe anasema juu ya utimilifu wake.

Uponyaji wa kimungu umejikita katika Yesu (Luka 5:17). Wanafunzi waliponya tu na mara zote kwa jina la Yesu. Uponyaji wa kimungu ni nguvu ya Bwana Yesu Kristo kuponya wagonjwa na wanaoteseka katika kujibu maombi ya imani.

Nguvu inayoponya imewekwa katika kujibu sala (Marko 11:24; 9:23). Aina ile ile ya uponyaji wa kimungu ambao ulitekelezwa na Bwana mwenyewe wakati alipoponya viwete, waliopooza na vipofu ni aina ile ile ya uponyaji ambayo Aliahidi ingefuata wale wanaoamini (Marko 16:17, 18).

Mungu sio Bwana wa nafsi na roho tu, lakini pia ni Bwana wa mwili (1 Wakorintho 6:19, 20). Ukombozi wa Kristo, ambao 'tumenunuliwa kwa bei,' ni pamoja na mwili wa kawaida.

1. Uponyaji wa kimungu katika Agano la Kale alilopewa Israeli umeandikwa katika Kutoka 15:26. Iliahidi nini?

   ______________________________

   ______________________________

2. Utoaji wa Agano Jipya unasemwa na Yakobo. Je! Inalinganaje na ile ya Agano la Kale? (Yakobo 5:14, 15)

   ______________________________

3. Je! Tunawezaje kujua kuwa Mungu hajabadilika? (Yakobo1:17; Waebrania 13:8) ________________________

________________________________________________

4. Je! Isaya alitabiri nini katika Isaya 53:6-9? ____________

________________________________________________

5. Kulingana na andiko katika Mathayo 8:16, 17, unabii wa Isaya ulitimizwa kwa njia gani?____________________

________________________________________________

6. Mungu anafahamika kwa watu wake kwa majina saba ya mshikano ambayo Yehova-Rapha ni mojawapo. Je! Unaweza kutambua jina hili katika Kutoka 15:26? ______

________________________________________________

7. Je! Ni msaada gani unaofuatana na msamaha wa dhambi kulingana na Mathayo 9:5? __________________

________________________________________________

8. Ni ishara gani zinafuatana na wale wanaoamini? (Marko 16:17, 18) ________________________________

________________________________________________

9. Je! Kuna tofauti kati ya dhiki na magonjwa? Fafanua. ____

________________________________________________

________________________________________________

10. Yakobo anataja vitu vinne vya kufanya ikiwa wewe ni mgonjwa. Ni nini? (Yakobo 5:13, 14)

1.________________________________________

2.________________________________________

3.________________________________________

4.________________________________________

11. Je! Ni masharti gani yanayohitajika ili kuponywa? (Yakobo 1:6, 7; Luka 11:9) ____________________

________________________________________

12. Je! Sala ya imani itafanya nini kwa mwamini anapokuwa mgonjwa? (Yakobo 5:15) ____________________

________________________________________

## SURA YA 14
# KURUDI MARA YA PILI

Kuja mara ya pili kwa Yesu Kristo ndiyo tumaini la baraka la kanisa. Kila wakati tunaposhiriki Meza ya Bwana, tunafanya hivyo kwa kumkumbuka Kristo na kazi Yake ya ukombozi mpaka atakapokuja. Yesu anakuja tena kibinafsi, katika muundo unaoonekana halisi kama vile alivyokuja mara ya kwanza. Anaweza kuja wakati wowote na "wafu katika Kristo watafufuka kwanza: Basi sisi tulio hai na tuliobaki tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu kukutana na Bwana angani, na hivyo tutakuwa na Bwana milele." (1 Wathesalonike 4:16, 17)

1. Mbingu ni mahali pa aina gani? (Ufunuo 12:1-4) ______

   ______________________________________________

2. Kwa nini Yesu alirudi kwa Baba? (Yohana 14:2, 3) ______

   ______________________________________________

3. Alienda kwa njia gani? (Matendo 1:9) ______________

   ______________________________________________

4. Malaika walisema nini? (Matendo 1:10, 11) __________

   ______________________________________________

5. Je! Paulo anamaanisha nini katika 2 Wakorintho 5:6-8 kuhusu mwamini kufurahiya kuwepo kwa ufahamu pamoja na Kristo wakati wa kufa? ____________________

   ______________________________________________

6. Maelezo ya Ujio wa Pili kwa Bwana yamefafanuliwa katika 1 Wathesalonike 4:16, 17. Yaorodheshe hapa chini.

a. ____________________

b. ____________________

c. ____________________

d. ____________________

e. ____________________

f. ____________________

g. ____________________

h. ____________________

7. Ni nini kinachoweza kujulikana juu ya wakati wa kurudi kwa Kristo? (Mathayo 14:36) Kumbuka: Kwa mafunzo zaidi soma Mathayo 24 yote. ____________________

____________________

8. Wakati Kristo atakapokuja, itakuwa katika siri? (Mathayo 24:26, 27) ____________________

____________________

9. Kwa sababu hakuna mtu anayejua wakati Yesu atakuja tena, mtu anapaswa kujiahadhari na nini? (Mathayo 24:24) ____________________

____________________

Mtu anapaswa kuishije? (Mathayo 24:42, 44) ____________________

____________________

10. Tuna maneno gani ya kufarijiana?
(1 Wathesalonike 4:13-18) ______________________________

______________________________________________________

______________________________________________________

11. Soma Ufunuo 22:1-7.
a. Nini itakuwa kazi ya wale watakaoishi milele pamoja na Mungu mbinguni? ______________________________

______________________________________________________

b. Nini kitatokea kwa nuru mbinguni? __________________

______________________________________________________

S U R A   Y A   1 5

# HUKUMU

Wanadamu wote watakutana na Mungu uso kwa uso (Warumi 14:11). Wengine watakuwa wakitarajia wakati wengine watakuwa na woga. Wale wanaomjua Yesu kibinafsi watafurahi kukutana naye, maana kwao kukutana na Kristo kunamaanisha kuishi pamoja naye milele (Ufunuo 20:6). Watu ambao wamemkataa Kristo wataogopa kuonana na Mungu…kwa ajili kwao, kukutana huko kunamaanisha kujitenga naye milele (Ufunuo 22:15-20).

Hukumu kwa waumini itafanyika wakati wa kuja kwa Kristo, wakati ambao atakaa kwenye kiti Chake cha hukumu kuwalipa watu wake kulingana na kazi zao.

1. Baada ya mtu kufa, nini kitakachofuata? (Waebrania 9:27-29) ______________________________

   ______________________________________________

2. Je! Kuna yeyote anayeepuka hukumu?________________

   ______________________________________________

3. Je! Yohana alisema nini juu ya mwamini kuja katika hukumu? (Yohana 5:24-29) ________________________

   ______________________________________________

4. Wapi na lini mwamini anahukumiwa kwa dhambi zake? (Warumi 8:1; Yohana 5:24; Ufunuo 2:11) ____________

   ______________________________________________

5. Ni nani atakayejitokeza kwenye kiti cha hukumu cha Kristo?

   2 Wakorintho 5:10 ____________________

   Warumi 14:10____________________

6. Je! Ni vitendo gani kadhaa ambavyo mwamini anawajibika navyo?

   Mathayo 12:36 ____________________

   Warumi 2:16 ____________________

   1 Wakorintho 4:5 ____________________

   1 Wakorintho 3:11-15 ____________________

   Warumi 14:23 ____________________

7. Je! Paulo anasema nini kuhusu hukumu? (Warumi 5:12-18) ____________________

   ____________________

8. Kuna tofauti gani kati ya kiti cha hukumu cha Kristo na hukumu kuu ya kiti cha enzi? (2 Wakorintho 5:10; Ufunuo 20:6, 11-12) ____________________

   ____________________

9. Ni nani atakayejitokeza mbele ya hukumu kuu ya kiti cheupe cha enzi? (Ufunuo 20:11-15) ____________________

   ____________________

10. Je! Ni vitabu gani vinatumiwa kuhukumu katika uamuzi wa mwisho? (Ufunuo 20:12)____________________

    ____________________

11. Soma Yohana 5:25-30.

a. Hakimu ni nani? ______________________________

b. Je, nini kitatokea kwa wafu wakati wa hukumu? ____

______________________________________________

c. Ni aina gani ya kujitenga itafanyika wakati wa hukumu? (Soma Ufunuo 20:11-15) ________________

______________________________________________

d. Wale wanaomjua Kristo wanapata "kuvuka." Yesu anamaanisha nini? (Yohana 5:24)__________________

______________________________________________



Foursquare Missions Press © 2003